

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOMBE
MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA KAMATI YA WAKUU WA
IDARA (CMT) KILICHOKETI TAREHE 24/01/2022 KWENYE UKUMBI
WA MIKUTANO WA HALMASHAURI.**

KUMB NA.06 /CMT/2021/2022/23– MAHUDHURIO.

WAJUMBE WALIOHUDHURIA:-

- | | | |
|--------------------------|-------|---|
| 1. Lutengano G. Mwalwiba | – | Mkurugenzi Mtendaji (W) - Mwenyekiti |
| 2. Majaga Tandasi | – | Kaimu Afisa Utumishi (W) - Katibu |
| 3. Honorat Mtasingwa | – | Afisa Utumishi |
| 4. Stanley Kabelinde | – | Kaimu Mweka Hazina (W) |
| 5. Sylvia Rwehabura | – | Afisa Mipango (W) |
| 6. Rashid S.Omary | – | Kny, Afisa Mifugo na Uvuvi (W) |
| 7. Gervas Magashi | – | Afisa ardhi na Maliasili (W) |
| 8. Harun A. N. Fashe | – | Kaimu Mhandisi Ujenzi (W) |
| 9. Yusuph Mwaipalu | – | Kaimu Afisa Uchaguzi (W) |
| 10. Kassim Mussa | – | Kny,Afisa Elimu Msingi (W) |
| 11. Steven Shilemba | –Kny, | Afisa kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W) |
| 12. Daniel Tesha | – | Kny,Mwanasheria wa Halmashauri (W) |
| 13. Sadi H. Kambi | – | Afisa TEHAMA |
| 14. Sungura M. F | – | Katibu TSC |
| 15. Kafiriti Amoni W. | – | Afisa usitawi wa Jamii(W) |
| 16. Michael S.Serakikya | – | Afisa misitu |
| 17. Bernadetha Tehingisa | – | Kny, Afisa Maendeleo ya Jamii (W) |
| 18. Leonard Nkingwa | – | Kny,Afisa Elimu Sekondari (W) |
| 19. Seleman D. Kuhanda | – | Mthibiti Ubora wa Elimu (W) |
| 20. Obeid H. Moshi | – | Mkaguzi wa ndani (W) |
| 21. Atupakisye Martin | – | Kaimu Mkuu wa kitengo cha habari (W) |
| 22. Dafosa Shayo | – | Afisa Nyuki (W) |
| 23. Mwita S. J. | – | Mkuu wa Kitengo cha manunuzi (W) |
| 24. Idrisa B. Kheri | – | Mwandishi wa vikao |
| 25. Joshua Makenza | – | Sekretarieti |
| 26. Petro Lugwisha | – | Mwandishi wa Vikao. |

KUMB NA.06/CMT/2021/2022/24 – WAJUMBE WASIOHUDHURIA:

- | | | |
|---------------------|---|--------------------------------|
| 1. Dr. Olden Ngassa | – | Mganga Mkuu (W) - Kwa taarifa. |
|---------------------|---|--------------------------------|

KUMB NA.06/CMT/2021/2022/25 – KUFUNGUA KIKAO.

Katibu kabla ya kumkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao alimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwajalia wajumbe uzima na afya njema. Baada ya hapo Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao.

Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 9.40 Arasili.

KUMB NA.06/CMT/2021/2022/26 – KURIDHIA AGENDA.

Katibu wa kikao alisoma agenda za kikao na kupokelewa na wajumbe. Baada ya hapo wajumbe waliridhia agenda zote kama zilivyowasilishwa.

KUMB. NA.06/CMT/2021/2022/27 – KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 5/11/2022.

Muhtasari husika ulisomwa mbele ya kikao na kupokelewa na wajumbe. Baada ya hapo Muhtasari ulitiwa saini na Mwenyekiti na Katibu kuwa kumbukumbu sahihi ya kikao cha tarehe 5/11/2022.

KUMB.NA.06/CMT/2021/2022/28 – YATOKANAYO NA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 5/11/2022.

Taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya kikao cha 5/11/2022 iliwasilishwa mbele ya kikao na kupokelewa na wajumbe. Baada ya hapo hapakuwa na hoja.

KUMB. NA.06/CMT/2021/2022/29 – TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KUISHIA 31/12/2021.

Taarifa iliwasilishwa mbele ya kikao na kupokelewa na wajumbe. Taarifa hiyo ilibainisha kuwa hadi kufikia tarehe 31/12/2021 Halmashauri ilikusanya jumla ya Tsh. 967,701,224.54 ikiwa ni sawa na 30.60% ya makisio ya mapato ya ndani kwa mwaka na Tsh.15,309,405,378.39 sawa na 44.50% ya makisio ya mapato yote kwa mwaka.

Pia Halmashauri kwa kipindi cha kuishia tarehe 31/12/2021 ilitumia jumla ya Tsh. 12,456,973,285.00 ikiwa ni sawa na asilimia 35.92%. Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuijadili ukurasa kwa ukurasa. Wajumbe walipitia vyanzo vyote vya mapato na kukubaliana makundi yote ya ukusanyaji wa mapato yaongeze kasi ya kukusanya mapato ili kuweza kufikia malengo ya mwaka.

Baada ya hapo wajumbe walipitisha taarifa ya mapato na matumizi kuishia tarehe 31 Desemba, 2021.

KUMB. NA.06/CMT/2021/2022/30 – TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ROBO YA PILI 2021/2022.

Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo robo ya pili 2021/2022 iliwasilishwa mbele ya kikao na kupokelewa na wajumbe. Taarifa hiyo ilikuwa katika makundi yafuatayo;-

- 1. Utekelezaji wa Fedha za bakaa zilizovuka mwaka wa fedha 2020/2021.** Tarifa ilionesha kuwa wakati mwaka wa fedha 2020/2021 unaisha jumla ya shilingi 574,022,072.82 zilivuka mwaka na kuingia mwaka 2021/2022 na pia hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2021 jumla ya Tsh. 280,596,078.60 zilikuwa zimetumika sawa na asilimia 48.88.

2. Mapokezi ya fedha za shughuli za maendeleo kwa kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2021/2022.

Kikao kilipokea taarifa kuwa Halmashauri ilipanga kutumia kiasi cha Tsh.10, 361,785,500.00 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za miradi ya maendeleo katika sekta mbalimbali ambazo zinajumuisha mapato ya ndani (40%) Tsh.923,348,000.00, wahisani Tsh.6,139,535,000.00 na Serikali kuu Tsh.3,298,902,500.00. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2021 Halmashauri ilikuwa imepokea kiasi cha Tsh.4,385,611,329.49 sawa na asilimia 42.32 ya fedha zilizopangwa kwa mwaka mzima ambazo ni Tsh.10,361,785,500.00. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2021 jumla ya Tsh. 3,404,724,770.65 zilitumika sawa na asilimia 77.63

3. Mapokezi ya fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka Serikali kuu na wahisani 2021/2022 kiasi cha Tsh. 1,318,548,360.00.

Kikao kilipokea taarifa kuwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ilipanga kutumia kiasi cha Tsh.3,298,902,500.00 kutoka Serikali kuu na fedha kiasi cha Tsh.6,139,535,000.00 kutoka kwa wahisani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta za Elimu msingi, Elimu Sekondari na Afya. Hadi hivi sasa Halmashauri imepokea kiasi cha Tsh. 730,646,000.00 kutoka Serikali kuu na kiasi cha Tsh. 587,902 360.00 kutoka kwa wahisani.

4. Mapokezi ya Fedha kiasi cha Tsh.55, 646,000.00 kutoka mfuko wa Jimbo.

Kikao kilipokea taarifa kuwa Halmashauri ilitenga kiasi cha Tsh.55,646,000.00 kutoka kwenye fedha za mfuko wa Jimbo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2021 fedha zote zilikuwa zimepokelewa na kupangiwa matumizi na kamati ya mfuko wa Jimbo.

Wajumbe walipokea taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuipitia ukurasa kwa ukurasa. Wakijadili taarifa hiyo, Afisa Mipango (W) alitoa taarifa kuwa miradi ya ujenzi wa kituo cha afya Bufanka, kituo cha afya Namonge na ujenzi wa kiwanda cha kuchakata na kufungasha mazao ya nyuki iko nje ya muda, alipendekeza Mhandisi wa ujenzi wa wilaya kuwa anatoa taarifa kwa Mkurugenzi Mtendaji (W) kila siku juu ya ujenzi unaoendelea. Wajumbe waliafiki ushauri huo na kuazimia kwa pamoja kuwa;

Azmio

- Ujenzi wa kituo cha afya Bufanka ukamilike ifikapo tarehe 15/02/2022.

- Ujenzi wa miradi ya afya kwa kutumia fedha za SWASH ikamilike ifikapo tarehe 15/02/2022.
- Ujenzi wa vyumba vya madarasa shule ya Sekondari Ng'anzo ukamilike ifikapo tarehe 30/04/2022.
- Uanzishwaji wa kampuni Tanzu ya Halmashauri ukamilike ndani ya wiki mbili kuanzia tarehe 24 Januari, 2022.

Baada ya hapo mthibiti ubora wa shule alitoa taarifa kuwa kuna shule za msingi saba hazina vyoo ikiwemo shule ya msingi Mbula. Alishauri taratibu za ujenzi wa vyoo kwenye shule hizo ufanyike haraka vinginevyo shule hizo zitafungwa kwa muda. Baada ya taarifa hiyo kutolewa kikao kiliazimia kuwa;

Azimio

- Taarifa ya hatua za ujenzi wa vyoo kwenye shule saba za msingi zisizo na vyoo ipelekwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W) baada ya wiki moja kuanzia tarehe 24 Januari, 2022.

Baada ya hapo wajumbe walijadili kuhusu Halmashauri kuunganisha umeme wa Generator ya Hospitali ya wilaya kwenda makao makuu ya Halmashauri kwa ajili ya matumizi ya kazi za ofisini mara inapotokea dharula ya kukatika umeme wa TANESCO. Katika majadiliano yaliyoendelea baadhi ya wajumbe walipendekeza kufanya matengenezo ya Generator zilizoko Makao Makuu ya Halmashauri. Hata hivyo ilionekana kuwa Generator za Halmashauri zinahitaji matengenezo makubwa kwa kuwa baadhi ya vifaa vilishang'olewa na kwamba tayari kuna taarifa ya ukaguzi wa Generator hizo ambayo inabainisha ubovu ulivyo na gharama za matengenezo. Katika majadiliano hayo baadhi ya wajumbe walipendekeza ukaguzi ufanyike upya kwa vile taarifa iliyopo ni ya zamani mno. Baada ya majadiliano ya muda mrefu wajumbe walikubaliana wataalam wapitie taarifa iliyopo ofisini na kufanya malinganisho ya gharama za matengenezo ya Generator hizo na bajeti ya fedha iliyopo.

5. Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya UVIKO – 19 kupitiza fedha za IMF

Afisa Mipango (W) aliwasilisha utekelezaji wa miradi ya UVIKO – 19 kupitia fedha za (IMF) iliyotekelezwa kwa kutumia njia ya manunuzi "force account" kama ilivyoelekezwa kwenye kikao cha kamati ya fedha cha tarehe 12/11/2021, Alisema kuwa Halmashauri ilipokea kiasi cha fasha Tsh. 2,530,000,000/= kwa ajili ya;

- Ujenzi wa madarasa 64 katika Idara ya Elimu Sekondari thamani ya Tsh.1,280,000,000/=.
- Ujenzi wa madara 43 katika Idara ya Elimu Msingi thamani ya Tsh.860,000,000/=.
- Ujenzi wa jengo la dharua katika Hospitali ya Wilaya Tsh. 300,000,000/=

- Ujenzi wa jengo la mtumishi "three in one" katika kituo cha Afya Bufanka Tsh.90,000,000/=.

Utekelezaji wake ni kama ifutatavyo;

- Madarasa yote ya shule za msingi na sekondari yamekamiliwa kwa mchanganuo ufuatao;

A. SHULE ZA SEKONDARI

NA	JINA LA SHULE	KIASI KILICHOPOKELEWA	KIASI KILICHOTUMIKA
1	BUSINDA S.S	120,000,000.00	120,000,000.00
2	NAMONGE S.S	120,000,000.00	120,000,000.00
3	LYAMBAMGONGO S.S	40,000,000.00	40,000,000.00
4	MSASA S.S	120,000,000.00	120,000,000.00
5	KATOME S.S	20,000,000.00	20,000,000.00
6	KATENTE S.S	160,000,000.00	160,000,000.00
7	BUSONGE S.S	80,000,000.00	80,000,000.00
8	BUTINZYA S.S	40,000,000.00	40,000,000.00
9	USIROMBO S.S	40,000,000.00	40,000,000.00
10	BUSONZO S.S	40,000,000.00	40,000,000.00
11	UYOVU S.S	120,000,000.00	120,000,000.00
12	RUNZEWE S.S	120,000,000.00	120,000,000.00
13	MSONGA S.S	120,000,000.00	120,000,000.00
14	BUKOMBE S.S	40,000,000.00	40,000,000.00
15	DOTTO BITEKO S.S	40,000,000.00	40,000,000.00
16	BULEGA S.S	40,000,000.00	40,000,000.00
17	IYOGELO S.S	20,000,000.00	20,000,000.00
	JUMLA	1,280,000,000.00	1,280,000,000.00

B. SHULE ZA MSINGI

NA	JINA LA SHULE	KIASI KILICHOPOKELEWA	KIASI KILICHOTUMIKA
1	LWAMKONGA	40,000,000.00	40,000,000.00
2	MKANGE - BUGELENGA	40,000,000.00	40,000,000.00
3	IPONYANZALA/BUTINZYA	40,000,000.00	40,000,000.00
4	MIGAMBA SHIKIZI	40,000,000.00	40,000,000.00
5	ISABILO S.M	60,000,000.00	60,000,000.00
6	IDOSELO S.M	200,000,000.00	200,000,000.00
7	KALILAMUYAYE S.M	40,000,000.00	40,000,000.00
8	NAMSEGA S.M	100,000,000.00	100,000,000.00
9	MTUKULA S.M	200,000,000.00	200,000,000.00
10	NYAMAGANA	100,000,000.00	100,000,000.00
	JUMLA	860,000,000.00	860,000,000.00

- Majengo ya dharura na jengo la mtumishi yapo katika hatua ya manunuzi, kwa sababu maelekezo yake ilikuwa yajengwe na mkandarasi baadaye maelekezo yalibadilika yajengwe kwa "Force Account".

Baada ya hapo kikao kilipitisha taarifa ya miradi ya maendeleo kama ilivyowasilishwa.

KUMB. NA. 06/CMT/2021/2022/31 – TAARIFA YA MKAGUZI WA NDANI ROBO YA PILI 2021/2022.

Taarifa ya Mkaguzi wa ndani iliwasilishwa mbele ya kikao na kupokelewa na wajumbe. Baada ya hapo wajumbe walipitia taarifa hiyo ukurasa kwa ukurasa na kusisitiza hoja zote zijibiwe na kufungwa. Pia Afisa Mipango, Mweka Hazina na Mkaguzi wa ndani wakae pamoja kujibu hoja ya ununuzi wa mchanga uliotumika kufyatulia matofali ya block pasipokutumia risiti ya mashine za kielektroniki. Vile vile, kikao kilipokea taarifa kuwa taratibu za ununuzi wa gari mpya zimekamiliwa kinachosubiriwa sasa ni kupata fedha kiasi cha shilingi

4,000,000/= kwa ajili ya kulipia bima. Baada ya taarifa hiyo kikao kiliazimia kuwa;

Azimio.

- Fedha kiasi cha shilingi 4,000,000/= kwa ajili ya bima ya gari mpya ilipwe tarehe 4/02/2022 ili gari mpya ifuatwe Dar Es Salaam.

Hoja nyingine ilikuwa kutolipwa kwa makato ya mishahara ya watumishi kwenye kifungu cha 5000 na kupelekwa kwenye mifuko ya PSPF na NHIF, ambapo kikao kilijadili hoja hiyo na kuazimia kuwa;

Azimio

- Stahiki za watumishi wa kifungu cha 500 zilipwe kwa wakati kila mwezi.

KUMB. NA. 06/CMT/2021/2022/32 – TAARIFA YA KITENGO CHA SHERIA ROBO YA PILI 2021/2022.

Taarifa hiyo ilihusisha mashauri mawili ambayo ni;

- Kesi ya ardhi Na.81/2020 ya Salum Mohamed na wenzake kumi na tatu dhidi ya Afisa ardhi wilaya ya Bukombe, kesi ipo Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya Geita.
- Kesi Na.03/2019 ya Bw. Phinias Kalokola dhidi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi Mtendaji (W), kesi ipo Mahakama ya Rufaa kanda ya Mwanza.

Taarifa nyingine zilihusu;

- Mabaraza ya kata na Sheria Ndogo za Halmashauri na Sheria Ndogo za vijiji.

Baada ya hapo kikao kiliidhinisha viwango vya tozo vitakavyokuwa vinatumika kwenye mabaraza yote ya kata katika eneo la Halmashauri kama ifuatavyo;-

1. Kufungua shauri - Tsh. 10,000/=.
2. Kupata nakala ya hukumu - Tsh. 2,000/=
3. Baraza kutembelea eneo la mgogoro kwenye madai ya ardhi - Tsh. 20,000/= kila upande.
4. Kupeleka jalada asilia kwenye Baraza la ardhi na nyumba la Wilaya Geita kwa ajili ya rufaa - Tsh. 20,000/=
5. Faini kwa makosa mbalimbali - Tsh.10, 000/=.
6. Huduma nyingine ambazo hazikuainishwa Tsh.3, 000/= kwa huduma.

Baada ya hapo taarifa ilipitishwa.

KUMB. NA.06/CMT/2021/2022/33 – TAARIFA YA MANUNUZI ROBO YA PILI 2021/2022.

Taarifa iliwasilishwa mbele ya kikao na kupokelewa na wajumbe. Taarifa hiyo ilibainisha kuwa katika kipindi cha robo ya pili 2021/2022 jumla ya shilingi 1,357,625,732/= zilitumika katika manunuzi ya vifaa, huduma zisizo za kitaalam kwa Idara zote na vitengo vyake katika Halmashauri. Wajumbe walipitia taarifa hiyo ukurasa kwa ukurasa na kuipitisha kama ilivyowasilishwa.

KUMB. NA.06/CMT/2021/2022/34 – TAARIFA YA UTAWALA MWEZI DESEMBA 2021.

Kaimu Afisa Utumishi (W) aliwasilisha taarifa ya Utawala kuishia tarehe 31 Desemba, 2021 na kupokelewa na wajumbe.

Taarifa hiyo ilibainisha mambo yafuatayo;-

1. Idadi ya watumishi

Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe hadi kufikia Desemba, 2021 ilikuwa na jumla ya watumishi 2,177 kati ya watumishi 2,622 wanaohitajika, hivyo kuwa na upungufu wa watumishi 445 kwa mujibu wa Ikama.

2. Maeneo ya Utawala

Hadi kufikia mwezi Desemba, 2021 maeneo ya Utawala yalikuwa kama yalivyotangazwa katika notisi ya mgawanyo wa maeneo ya Utawala katika Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Mji) na amri ya mgawanyo wa maeneo ya Utawala katika Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) mwaka 2019.

3. Taarifa mbalimbali.

Taarifa zilizowasilishwa ni;-

▪ **Taarifa kuhusu watumishi waliohama/kuhamia.**

Kikao kilipokea taarifa kuwa mtumishi ndugu Daudi L. Kanana (Msaidizi wa Hesabu) amehamia Halmashauri ya Wilaya ya Geita kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe na mtumishi ndugu Asifiwe B. Mjujulu (Afisa Mifugo) amehamia Bodi ya nyama Dar Es Salaam.

▪ **Mashauri ya kinidhamu.**

Mashauri ya kinidhamu yalikuwa matatu ambayo yaliwahusu watumishi wafuatao;

1. Stanley Bushiri (Fundi sanifu) – Kosa la utoro kazini.
2. Mary S. Mgulla (Muuguzi) – Tuhuma ya wizi wa dawa.
3. Erick A. Ngongi (Msaidizi Mimitu 1) – Kosa la Uhujumu Uchumi.

Baada ya hapo taarifa ilipitishwa.

KUMB NA.06/CMT/2021/2022/35 – KUPITIA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA,UONGOZI NA MIPANGO WA TAREHE 17/12/2021 PAMOJA NA YATOKANAYO YAKE.

Muhtasari husika ulisomwa mbele ya kikao na kupokelewa na wajumbe na kufanyiwa marekebisha kadhaa. Baada ya hapo wajumbe walijadili taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya kikao husika na kuruhusu taratibu za kuandaa makabrasha ya kikao ziendelee.

KUMB NA.06/CMT/2021/2022/36 – MAAGIZO YA SERIKALI.

Maagizo ya Serikali hayakuwepo.

KUMB NA.06/CMT/2021/2022/37 – KUFUNGA KIKAO.

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kufunga kikao baada ya dondoo zote kujadiliwa na kumalizika.

Mwenyekiti kabla ya kufunga kikao aliwashukuru wajumbe kwa ushiriki wao katika kikao hicho. Baada ya hapo Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 2.47 usiku.

"UMETHIBITISHWA"

MWENYEKITI

KATIBU

JINA *GERVAS MAGASHI*

JINA *MAJAGA TRADASI*

SAINI *[Signature]*

SAINI *[Signature]*

TAREHE *03.03.2022*

TAREHE *03.03.2022*

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
BUKOMBE.